


Eastern Africa Journal of Kiswahili

[ISSN 2958-1036]
Volume: 05 Issue: 01 | May-2026

EAJK

# Nafasi ya Kiswahili katika Ujenzi wa Utamaduni wa Uongozi katika Shule ya Msingi ya Mungakha, Kaunti ya Kakamega, Kenya

**Authors**

**Stephen Muyundo Ndinyo [1]; Ernest Sangai Mohochi [2]**

**Main author's email: muyundos@gmail.com**

**(1.2) Kibabii University, Kenya.**

**Cite this article in APA**

Ndinyo, S. M., & Mohochi, E. S. (2026). Nafasi ya Kiswahili katika ujenzi wa utamaduni wa uongozi katika shule ya msingi ya mungakha, kaunti ya kakamega, kenya. *Eastern Africa journal of Kiswahili,* 5(1), 42-53. https://doi.org/10.51317/eajk.v5i1.977

OPEN ACCESS A publication of Editon Consortium Publishing (online)

**Article history**
Received: 2026-03-21
Accepted: 2026-04-15
Published: 2026-05-07

Scan this QR to read the paper online

**Copyright:** ©2026 by the author(s). This article is an Open Access article distributed under the terms and conditions of the Creative Commons Attribution-NonCommercial-ShareAlike 4.0 International License (CC BY-NC-SA 4.0).

**Ikisiri**

Lengo la makala haya ni kupambanua nafasi ya Kiswahili katika ujenzi wa utamaduni wa uongozi katika Shule ya Msingi ya Mungakha, Kaunti ya Kakamega, nchini Kenya. Uongozi wa kufana hujengeka kwa tamaduni zinazokubalika na zenye kuheshimika. Makala haya yalipambanua nafasi ya Kiswahili katika ujenzi wa utamaduni wa uongozi katika Shule ya Msingi ya Mungakha, Kaunti ya Kakamega, nchini Kenya. Malengo mahususi yalikuwa ni: Kutathmini utamaduni wa uongozi wa shule; kubainisha ni jinsi gani Kiswahili kinatumika kujenga utamaduni wa uongozi wa shule; na kupambanua mitazamo ya washikadau kuhusu matumizi ya Kiswahili katika uongozi wa Shule ya Msingi ya Mungakha. Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Tabia ya Uongozi ya Fleenor (2006). Mkabala wa kithamano na muundo wa kimfano uliongoza utafiti huu. Mbinu ya ukusanyaji wa data iliyotumiwa ni hojaji. Sampuli lengwa ilihusisha shule moja ya msingi, mwalimu mkuu, naibu wake, wakuu wa jopo, viranja, wanachama wa halmashauri ya uongozi wa shule, wafanyakazi na wazazi. Usampulishaji wa kimaksudi uliteua Shule ya Msingi ya Mungakha, mwalimu mkuu na naibu wake. Usampulishaji wa kinasibu uliwachagua wanachama wa halmashauri ya usimamizi wa shule, wakuu wa jopo, viranja na wafanyakazi. Data iliyokusanywa ilichanganuliwa kwa kutumia kielelezo cha nyaraka, kisha ikawasilishwa kwa kurejelea malengo ya utafiti kwa maelezo ya kifafanuzi na mijadala kutolewa. Matokeo yalibainisha kuwa utamaduni katika Shule ya Msingi ya Mungakha ulikuwa wa umoja, uongozi wa kielelezo, mazingira bora ya ujifunzaji, ugatuzi wa mamlaka, kushirikishwa kwa wanafunzi, kuhusishwa kwa wazazi na mawasiliano ya wazi. Lugha ya Kiswahili na Kiingereza zilitumika kwa kiwango kizuri huku Kinyala kikitumika kwa kiwango cha chini. Washikadau walipendelea matumizi ya lugha ya Kiswahili na Kiingereza kwa kiwango cha wastani na Kinyala kwa kiwango cha chini sana katika shule hii.

**Maneno muhimu:** Kiswahili, lugha, ujenzi, uongozi na utamaduni.

**UTANGULIZI**

Uongozi katika taasisi yoyote ile ni muhimu na huchangia fanaka katika kuyafikia malengo ya taasisi husika. Lugha, ambayo huchangia katika ujenzi wa uongozi, ni mojawapo ya nguzo muhimu sana katika kuyafikia malengo ya taasisi yoyote ile. Uongozi wa kupigiwa mfano hujengeka kwa tamaduni zinazoshikiliwa na kurejelewa na kila mmoja katika taasisi. Uongozi ni kipengele muhimu cha kila shirika na hivyo basi hakuna shirika linaloweza kuwepo bila kiongozi (Aibieyi, 2014). Lugha ni mojawapo ya kipengele muhimu katika utamaduni wowote ule, hususan katika kuukuza na kuuendeleza. Kiongozi katika taasisi yoyote ni sharti awe na uwezo wa kutekeleza malengo ya taasisi husika. Hivyo basi, ni sharti kiongozi awe na uwezo na utashi wa kuwaunganisha watu katika taasisi husika ili kuyafikia malengo yake na matumizi mema ya lugha ni moja kati ya sifa muhimu anazopaswa kuwa nazo.

Hongboontri na Keawkhong (2014) wanashikilia kuwa tamaduni za shule ni za kipekee na tofauti ambazo huundwa, kuvunjwa na kuundwa upya na watu wanaochukuliwa kuwa sehemu ya taasisi kama vile walimu, wanafunzi, wazazi na jamii miongoni mwa wengine wengi. Utamaduni katika shule ni jinsi walimu na wanafunzi wanavyokabili maisha katika mazingira ya shule kwa njia inayokubalika na kuheshimiwa na wote. Kila taasisi ya elimu huwa na imani, maadili, sheria na desturi zinazokubalika kutokana na tajriba za wenyeji wa taasisi mbalimbali wanapokabiliana na masuala tofauti. Widodo (2019) anashikilia kwamba utamaduni wa shule ni raslimali ya kimsingi ya kuafikia kikamilifu malengo ya elimu katika shule hiyo.

Usman na Yusrizal (2016) wanaeleza kuwa utamaduni wa shule ni nguzo ya ufanisi wa shule katika kutekeleza mchakato wa kujifunza. Ni sifa maalum zinazotofautisha taasisi moja na nyingine katika shughuli za kila siku. Ili kufanikisha shughuli mbalimbali za taasisi za elimu ni vyema kuwa na tamaduni zinazokubalika na kurejelewa na kila mmoja katika taasisi hiyo. Santri (2016) anaeleza kwamba utamaduni chanya unaweza kutoa fursa za mawazo ambayo yanaweza kuboresha utendakazi wa walimu na kusaidia katika kuunda utamaduni bora wa shule.

Vile vile, Barkman (2015) anasema kuwa kiongozi yeyote yule huwa na nguvu na udhaifu wake. Viongozi wenye ufanisi katika shule hulenga kuelekeza walimu na wanafunzi huku utendakazi wao ukiwa wa kitaaluma katika shughuli zao za kila siku. Uongozi wa kila taasisi hujikita kwa mtindo wa kiongozi katika kuendesha shughuli mbalimbali katika taasisi yake. Mtindo huo hutabirika mara kwa mara kwenye taasisi na hivyo baada ya muda huwa ni mojawapo ya tamaduni katika uongozi wake. Katika taasisi yoyote ile lugha ni mojawapo ya kiambajengo kikubwa kinachotumika katika kuendeleza utamaduni.

Shule yeyote ile ni sharti iwe na uongozi dhabiti ndiposa iweze kunawiri. Uongozi huo hujengeka kwa utamaduni imara unaokuzwa na kuendelezwa kila uchao. Lugha ya Kiswahili ilikuwa mojawapo ya mihimili ya kimsingi ya ujenzi na ukuaji wa utamaduni huu imara wa uongozi. Uongozi wa Shule ya Msingi ya Mungakha kwa muktadha wa makala haya ulihusisha mwalimu mkuu, naibu wake, wakuu wa majopo, viranja na bodi ya halmashauri ya shule.

Kufikia hapa ni vyema kutambua ya kwamba, sawa na kazi hii wataalam waliorejelewa awali wamejikita katika suala la uongozi na utamaduni lakini hawajarejelea nafasi ya lugha hasa ya Kiswahili katika ujenzi wa utamaduni wa uongozi wa shule. Hivyo basi, makala haya yaliangazia nafasi ya Kiswahili katika ujenzi wa utamaduni wa uongozi katika Shule ya Msingi ya Mungakha katika Kaunti ya Kakamega, Kenya. Malengo mahususi ya kazi hii yalikuwa ni: Kutathmini utamaduni wa uongozi katika Shule ya Msingi ya Mungakha; kubainisha jinsi Kiswahili kinatumika kujenga utamaduni wa uongozi wa Shule ya Msingi ya Mungakha na kupambanua mitazamo ya washikadau kuhusu matumizi ya Kiswahili katika uongozi wa Shule ya Msingi ya Mungakha. Umuhimu wa utafiti huu ni kubainisha nafasi ya lugha ya Kiswahili katika kujenga na kuendeleza utamaduni wa uongozi katika taasisi za elimu. Makala haya yamegawika katika sehemu sita: Sehemu ya utangulizi, uhakiki wa maandishi, mbinu za utafiti, uwasilishaji wa matokeo pamoja na hitimisho na mapendekezo.

**MAPITIO YA MAANDISHI**

**Ujenzi wa Utamaduni wa Uongozi katika Taasisi za Elimu**

Utamaduni wowote ule wa uongozi katika taasisi yoyote ile ni sharti ujengwe na kuendelezwa. Mwakale (2017) alishughulikia uongozi na utamaduni wa ubora

katika vyuo vikuu vya kibinafsi nchini Kenya: Mfano wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Kimataifa cha Marist. Matokeo yake yalionyesha kuwa kujitolea kwa uongozi kuliathiri uundaji wa utamaduni bora wa kazi, uwepo wa viongozi wa kupigiwa mfano ulikuwa muhimu katika kuendeleza utamaduni wa uongozi, kuhusishwa kwa washikadau pia kulikuwa muhimu sana katika ukuzaji wa utamaduni wa uongozi hasa walipohusishwa katika kuafikia maamuzi mbalimbali. Mawasiliano nayo yalijitokeza kuwa kigezo muhimu kwa ukuzaji wa utamaduni bora; ilibainika kuwa ni sharti kuwe na njia wazi na thabiti katika kupitisha ujumbe bora kama njia ya kuhakikisha mazoea ya ubora yanazingatiwa. Hatimaye, changamoto za ukuzaji wa utamaduni bora kama vile ukosefu wa fedha, ukosefu wa kujitolea kwa wasimamizi wakuu, tofauti za utamaduni wa viongozi baina ya wasimamizi wakuu, kupinga mabadiliko na kuwepo kwa viongozi wenye tamaa na nia ya kujifaidisha kutoka katika nafasi zao zilibainika (Mwakale, 2017). Masuala ya uongozi na utamaduni yalilengwa pia katika kazi kwa kujikita katika nafasi ya Kiswahili katika ujenzi wake.

Block (2003), katika kuchunguza uhusiano wa uongozi na utamaduni, alitathmini hali ya uhusiano kati ya uongozi na utamaduni katika taasisi na shirika la kibinafsi la mauzo. Ilibainika wazi kuwa mtindo wa uongozi wa msimamizi ulihusiana pakubwa na mitazamo ya wafanyakazi anaowasimamia kuhusu utamaduni wa taasisi (Block, 2003). Wasimamizi wenye viwango vya juu vya sifa ya uongozi wenye mabadiliko walihusishwa na viwango vya juu vya misheni, mabadiliko na uthabiti katika mashirika yao. Wasimamizi walikuwa na ushawishi mkubwa sana kwa waliowasimamia moja kwa moja katika mitazamo ya utamaduni wa taasisi kuliko wasimamizi wa viwango vingine vyote visivyo vya moja kwa moja katika taasisi. Hivyo basi, utamaduni wa uongozi ni kipengele muhimu cha shirika zima katika karne hii ya ishirini na moja.

Xenikou (2022), akiangazia uongozi na utamaduni katika taasisi, anashikilia kwamba katika taasisi utamaduni unapaswa kuwa na imani na kanuni za tabia kwa kurejelea jinsi unavyowaelekeza wafanyakazi. Waasisi wa taasisi na timu zao wana nafasi kubwa katika ukuzaji wa utamaduni wa taasisi zao kwa vile huwa na sifa ya imani dhabiti kuhusu maamuzi wanayoyachukua ili taasisi zao zifanikiwe na kubadilika ili zistawi (Xenikou, 2022). Waasisi na viongozi wengine huwa na njia mbalimbali za kuwasiliana, kuanzisha na kuimarisha maadili kama vile kuwa na mifano ya kuigwa, ukufunzi, tuzo na kupandishwa vyeo. Vilevile, viongozi wanaweza kutumia mbinu tofauti katika kukuza nafasi za kubadilika kwa utamaduni kama vile kupandishwa madaraka kwa wafanyakazi kutoka tamaduni tofauti, kuajiri wafanyakazi wengine kutoka nje na kushirikisha teknolojia katika taasisi. Msomi Xenikou (2022) anasema kwamba kushiriki huhusiana moja kwa moja na ukuaji wa kibinafsi wa taasisi ili kuafikia utendakazi wa kiwango cha juu na kukuza maslahi ya wafanyakazi.

Daoud na Tarek (2023) wanashikilia kuwa ni jukumu la uongozi kufanikisha mabadiliko katika utamaduni na viongozi wenye ufanisi hutumia mbinu mbalimbali kuafikia hili. Uongozi hujitokeza kama msukumo unaoongoza uundaji, mabadiliko na uhifadhi wa utamaduni. Viongozi huwa na jukumu muhimu katika kuwa mifano ya kuigwa, kutoa maono na mwelekeo, mawasiliano na uratibu, uwezeshaji, uwajibikaji, kuhakikisha kuwepo kwa raslimali za kutosha kwa wafanyakazi na mwongozo kwa wafanyakazi (Daoud & Tarek, 2023). Tabia na matendo ya uongozi hutumika kama kiunzi ambacho ni kanuni za kitamaduni na kimaadili.

**Matumizi ya Lugha katika Ujenzi wa Utamaduni wa Uongozi**

Utamaduni wa uongozi ni muhimu sana katika kukuza na kuendeleza taasisi yoyote ile. Utamaduni huu hukuzwa na kuendelezwa na vipengele mbalimbali. Lugha ni mojawapo ya kiambajengo muhimu cha utamaduni wowote ule. Kwa mujibu wa utafiti wa Case et al. (2017), ilibainika wazi kuwa ilikuwa vigumu kwa wazawa wazungumzaji wa lugha asilia ya Lao kupata maneno ya kuelezea uongozi au vyeo vya viongozi nje ya muktadha wa kisemantiki na kijamii uliodhinishwa rasmi. Matokeo makuu yaliyobainika ni kuwa kwa mtazamo wa Chama cha Mapinduzi cha watu wa Lao, mamlaka na uongozi ni dhana moja (Case et al., 2017). Hali hii ya kijamii inajitokeza kuwa kizuizi cha kiisimu kwa kile kinachoweza na kisichoweza kuelezwa kama uongozi kule Laos (Case et al., 2017). Ukosefu wa maneno haya ya uongozi katika jamii hii ya Lao kunaashiria utamaduni wao wa uongozi ambao haurejelei vyeo tofauti (Case et al., 2017).

Souba na Souba (2016) wanasema kwamba ugiligili wa maneno hutokana na mwenendo wa watu kusikia kile kinachowanufaisha, hivyo kuwa kizingiti cha mawasiliano katika lugha. Upungufu wa maneno ni muhimu kwa kurejelea uongozi kwa vile lugha ndiyo raslimali muhimu katika uongozi. Lugha yaweza kuwa mbali na ukamilifu, kukosa kueleweka, isiyo sahihi na isiyoeleweka (Souba et al., 2016). Ili kuwepo na ufanisi, viongozi lazima watambue kwamba lugha hujenga miktadha ambayo kiasilia ni funge. Kila shirika kimsingi zaidi ni mfumo wa mtandao changamano wa mazungumzo ya mara kwa mara yatokeayo kila siku. Utafiti huu ulibaini kwamba viongozi ni sharti wawe wazi na wapitishe ujumbe wao kwa kifupi iwezekanavyo (Souba et al., 2016). Pia, wanapaswa kuhimiza mazungumzo katika viwango tofauti vya shirika husika na kutumia lugha yenye kubadilika katika kuvumbua mustakabali mpya. Nafasi hii ya lugha ya Kiswahili ilibainika kuwa muhimu sana katika ujenzi wa utamaduni wa uongozi.

Buenviaje et al. (2017) walishughulikia matumizi ya lugha ya uongozi yenye kutia motisha na jinsi yalivyoathiri utendakazi wa wanakifakulteti katika taasisi mojawapo ya kibinafsi ya elimu kule Ufilipino. Matokeo ya kazi hiyo yalikuwa kwamba kulikuwa na kiwango kikubwa cha kusisitiza, kutoa mwelekeo na maana ili lugha ya kiongozi iwe ya kuwatia motisha wafanyakazi katika utendakazi wao kwenye kitivo. Watafitiwa walikuwa na imani kwamba walitiwa motisha ili kufanya kazi vyema zaidi kupitia kujulishwa habari kuhusu mafanikio ya shirika, hali ya kifedha na kutuzwa. Lugha nzuri ni ile inayotoa mwelekeo kwa kuwaeleza moja kwa moja kuwa usimamizi uliwaamini kwa kuwapa majukumu ya kiwango cha juu kama njia ya kuwatia motisha na hamu ya kufanya kazi (Buenviaje et al., 2017). Utafiti huu unadhibitisha kwamba, kwa mujibu wa Nadharia ya Lugha ya Umotishaji, wanakifakulteti walifanya kazi zao vyema kwa kuwasilishwa habari zinazohitajika moja kwa moja kutoka kwa mtendaji mkuu au wakurugenzi wa masomo katika taasisi ile (Buenviaje et al., 2017).

Tampubolon na Harati (2019) katika kazi yao waliangazia jukumu la utamaduni wa taasisi, mawasiliano na mtindo wa uongozi katika kuridhika kikazi katika shule za upili na shule za upili za kiufundi. Matokeo yalibainisha kwamba utamaduni wa uongozi ulikuwa wa kiwango cha chini katika kuridhika kikazi, huku mawasiliano yakiwa na athari kubwa mno kwa kuridhika kikazi. Aidha, mtindo wa uongozi ulikuwa na athari kubwa katika kuridhika kikazi (Tampubolon na mwenzake, 2019).

Kazi mbalimbali zimejadiliwa kwa kurejelea ujenzi wa utamaduni wa uongozi katika taasisi za elimu. Pengo linalotokea ni kwamba kazi hizi zilirejelea utamaduni na uongozi kwa jumla, matumizi mbalimbali ya lugha na viongozi na jukumu la uongozi katika kubadilisha utamaduni wa taasisi. Kinyume na kazi hizo, kazi hii iliangazia nafasi ya lugha ya Kiswahili katika ujenzi wa utamaduni wa uongozi.

**Mitazamo ya Washikadau kuhusu Matumizi ya Lugha katika Uongozi**

Washikadau wana nafasi kubwa katika kukuza na kuendeleza taasisi yoyote ile. Lugha ni mojawapo ya kiambajengo muhimu katika jamii kinachoangaziwa na washikadau tofauti katika jamii. Kwa mujibu wa Tembe na Norton (2008), wakishughulikia ukuzaji wa lugha za kiasili katika shule za msingi nchini Uganda kwa kurejelea jamii kama washikadau, jamii ilikuwa mojawapo ya washikadau wakubwa katika elimu ya lugha. Maoni ya jamii kama washikadau yalikuwa muhimu sana katika utekelezaji wenye ufanisi wa sera mpya ya lugha (Tembe na mwenzake, 2008). Sera hii mpya nchini Uganda ilikuwa ni kukuza ufundishaji wa lugha za kiasili kwa miaka ya kwanza minne katika shule ya msingi. Matokeo yalikuwa kwamba washikadau hawa, licha ya kufahamu sera hii mpya ya ufundishaji wa lugha asilia, hawakukubaliana na utekelezaji wa sera hii katika shule zao (Tembe et al., 2008).

Licha ya wao kutambua umuhimu wa lugha asilia katika kukuza utambulisho wao na katika ukuzaji wa utamaduni wao, kipaumbele cha juu kilikuwa ni maendeleo ya kielimu na matamanio ya watoto wao kuwa sehemu ya jamii kubwa ya kimataifa (Tembe na mwenzake, 2008). Zaidi ya hayo, lugha za kiasili kama vile Kiganda na Kiswahili zilizokuwa lugha za matumizi katika maeneo makubwa zilichukuliwa kuwa za manufaa kama lugha pana za mawasiliano. Kwa hakika, ni lugha ya Kiingereza ambayo ilipata uungwaji mkono kufundishwa katika shule za msingi na washikadau wengi (Tembe na mwenzake, 2008).

Misheck na Shoko (2013) walitafitia mitazamo ya washikadau kwa kurejelea utekelezaji wa sera ya lugha

ya ujifunzaji nchini Malawi. Matokeo ya kazi hii yalikuwa kwamba lugha iliyotumiwa kwa ufundishaji ilikuwa tofauti na lugha ya mama kwa asilimia tisini (90%) ya wanafunzi. Hii ndiyo hali halisi kwa vile washikadau wanaamini kwamba lugha yao ya taifa na lugha ya Kiingereza ni muhimu sana katika kutafuta ajira na kutahini wanafunzi katika mitihani ya kitaifa (Misheck na mwenzake, 2013). Hata hivyo, utafiti huu ulibaini kwamba wengi wa wanafunzi walioshiriki waliweza kusoma na kuandika kwa lugha ya Kichichewa na Kiingereza.

Mahamed (2015) alishughulikia mitazamo ya washikadau kuhusu lugha ya Kisomali kama nyenzo ya ufundishaji katika shule za msingi za umma katika eneo la Benadir, Mogadishu, Somalia. Matokeo ya utafiti huu yalikuwa kwamba asilimia hamsini na mbili (52%) ya wanafunzi walipendelea walimu wao kufundisha wakitumia Kisomali, huku asilimia thelathini na tisa (39%) wakipendelea Kiingereza na asilimia tisa (9%) wakipendelea lugha ya Kiarabu kutumika darasani (Mahamed, 2015). Pili, ilibainika kwamba asilimia themanini na tatu nukta moja (83.1%) ya walimu walitumia lugha ya Kisomali darasani kwa sababu ni lugha iliyoeleweka vyema na wanafunzi (Mahamed, 2015). Asilimia nane nukta saba (8.7%) ya walimu walitumia Kiingereza katika kufundisha darasani. Asilimia nane nukta mbili (8.2%) ilitumia lugha ya Kiarabu katika kufundisha (Mahamed, 2015). Hata hivyo, asilimia tisini na mbili nukta tano (92.5%) ya wazazi walipendelea lugha ya Kisomali kutumiwa nyumbani na shuleni. Asilimia tano (5%) ya wazazi walipendelea Kiingereza huku asilimia mbili (2%) ya wazazi wakipendelea lugha ya Kiarabu (Mahamed, 2015). Utafiti huu umetujengea msingi wa tofauti za mapendeleo ya washikadau tofauti pia yakiangaziwa kama ilivyo katika kazi hii kwa kurejelea nafasi ya Kiswahili katika ujenzi wa utamaduni wa uongozi.

Sehemu hii ilirejelea tafiti zilizofanywa kuhusu mitazamo ya washikadau kuhusu sera kuhusiana na lugha asilia, lugha ya ujifunzaji na lugha asilia kama nyenzo ya ujifunzaji katika taasisi za elimu. Tafiti hizi ziliangazia nafasi ya washikadau kuhusiana na lugha katika utekelezaji wa sera mbalimbali. Pengo lililodhihirika katika kazi hizi ni kwamba hazikurejelea mitazamo ya washikadau kuhusu matumizi ya Kiswahili katika uongozi.

**Nadharia ya Utafiti**

Makala haya yaliongozwa na Nadharia ya Tabia ya Uongozi (Trait Approach to Leadership) iliyoasisiswa na Thomas Carlyle mwaka wa 1841 na kuendelezwa na Allport (1936) na baadaye Fleenor (2006). Kwa mujibu wa Fleenor (2006), nadharia hii huangazia sifa binafsi za viongozi kama vile sifa za kimaumbile na za kibinafsi kama vile sifa za mtu, umahiri na maadili.

Nadharia hii ina mihimili minane (8) kama ifuatavyo: Kwanza, kiongozi awe msondani; pili, mwenye ufahamu na uwazi; tatu, mwenye uwajibikaji wa kiwango cha juu; nne, kiongozi awe mwezeshaji wa kuweka malengo katika taasisi; tano, mwenye umahiri mkubwa; sita, mwenye uwezo mzuri katika mawasiliano; saba, mwenye haiba ya juu na hatimaye, kiongozi mwenye ufanisi mkubwa. Kazi hii iliongozwa na mihimili hii yote ya Nadharia ya Tabia ya Uongozi. Uongozi ni nguzo muhimu katika taasisi yoyote ile katika ufanisi wake. Mhimili huu ulitumiwa kuchanganua data kuhusu nafasi ya Kiswahili katika ujenzi wa utamaduni wa uongozi katika Shule ya Msingi ya Mungakha.

**MBINU ZA UTAFITI**

Mkabala wa utafiti huu ulikuwa ni utafiti wa kithamano na muundo wa kimfano. Muundo huu huchukua idadi ndogo ya sampuli kubwa na huchunguzwa kwa kina ili kuelewa kundi ndogo la sampuli hiyo (Punch, 2013). Mbinu ya hojaji ilitumika kukusanya data kutoka kwa watafitiwa nyanjani. Hojaji mseto ilitumika kwa vile ilishirikisha maswali funge na maswali wazi kwa pamoja. Hojaji hii ilikuwa na sehemu tatu zilizosukwa kurejelea malengo matatu ya utafiti. Mseto huu wa maswali ulikuwa muhimu kukusanya data toshelevu kurejelea malengo ya utafiti.

Umma lengwa ulihusisha Shule ya Msingi ya Mungakha, mwalimu mkuu, naibu wake, wakuu wa jopo, walimu wa darasa, viranja, wafanyakazi na wanachama wa halmashauri ya shule. Usampulishaji wa kimaksudi ulitumika kuteua Shule ya Msingi ya Mungakha, mwalimu mkuu na naibu wake. Wawili hawa waliteuliwa kimaksudi kwa kuwa ndio viongozi wakuu katika shule hii. Usampulishaji wa kinasibu ulitumika katika kuwachagua wanachama wa halmashauri ya usimamizi wa shule, wakuu wa jopo, viranja na wafanyakazi. Usampulishaji huu ulihakikisha

nafasi sawa kwa watafitiwa na hivyo kupunguza mapendeleo katika kazi hii.

Sampuli ilihusisha viongozi wakuu wawili (2) kati ya watatu (3) ambao ni mwalimu mkuu na naibu wake waliowakilisha asilimia sitini na saba (67%). Wakuu wa jopo wanne (4) kati ya nane (8) waliowakilisha asilimia hamsini (50%), viranja nane (8) kati ya 22 waliowakilisha asilimia thelathini na sita (36%). Wafanyakazi watatu (3) kati ya watano (5) waliowakilisha asilimia sitini (60%) na wawakilishi wa halmashauri ya uongozi wa shule sita (6) kati ya kumi na tano (15) waliowakilisha asilimia arobaini (40%). Data iliyokusanywa ilichanganuliwa kwa kutumia kielelezo cha nyaraka na kuwasilishwa kwa kurejelea malengo ya utafiti kwa maelezo ya kifafanuzi na mijadala kutolewa. Kipimo cha Likert kilitumiwa katika kueleza kiwango cha matumizi ya Kiswahili katika Shule ya Msingi ya Mungakha. Tena, kipimo hiki kilikadiria mitazamo mbalimbali ya washikadau kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili katika Shule ya Msingi ya Mungakha.

## MATOKEO YA UTAFITI

Makala haya yamepambanua nafasi ya Kiswahili katika ujenzi wa utamaduni wa uongozi katika Shule ya Msingi ya Mungakha. Hii ni kwa kuangazia kwa kina tathmini ya utamaduni wa uongozi, matumizi ya Kiswahili katika kujenga utamaduni wa uongozi na mitazamo ya washikadau kuhusu matumizi ya Kiswahili katika ujenzi wa utamaduni wa uongozi wa Shule ya Msingi ya Mungakha kama ifuatavyo;

### Utamaduni wa Uongozi wa Shule ya Msingi ya Mungakha

Utamaduni wa uongozi uliojitokeza katika Shule hii ya Msingi ya Mungakha ulikuwa na sifa za umoja, uongozi wa kielelezo, mazingira bora ya ujifunzaji, kushirikisha wanafunzi, kuhusisha wazazi na mawasiliano mazuri. Utamaduni huu umejadiliwa kwa mapana kama ifuatavyo:

### Umoja

Hiki ni mojawapo ya kipengele cha utamaduni kinachojitokeza katika shule hii ya Msingi kwa kiwango kizuri sana. Ili kuwepo na maendeleo katika jamii, viongozi ni sharti waungane na wapate uungwaji mkono kamilifu na wanajamii (Nahame et al., 2015). Katika shule hii kuna umoja katika lengo kuu la kuwahudumia wanafunzi. Uongozi wa shule umewaleta pamoja walimu, wafanyakazi, wanafunzi na wanajamii. Wote hawa wanafanya kazi na kuishi kama jamii moja. Jamii katika shule hii imeungana na hakuna tofauti zozote za kitabaka, kikabila au kinyadhifa.

### Uongozi wa Kielelezo

Uongozi huu husukuma walimu, wafanyakazi na wanafunzi katika Shule hii ya Msingi ya Mungakha sana na kwa haraka katika kuyafikia malengo yao. Viongozi hawa hushiriki moja kwa moja katika kufanya kazi huku wakiongoza kwa mfano na kuweka matarajio ya juu. Viongozi ni sharti watambue umuhimu wa jukumu la kuwa kielelezo kama sehemu kuu katika mchakato wa kuunda utambulisho na kukuza wanaume na wanawake watakaoongoza baada yao (Sealy & Singh, 2008). Hii huwa dhahiri wazi kwa viongozi wa shule kama vile mwalimu mkuu kuongoza katika ufundishaji katika madarasa yake na viranja kuwa na nidhamu ya kiwango cha juu na kufanya vyema kwenye mitihani. Hali hii huwatia mshawasha walimu katika utendakazi wao. Aidha, wanafunzi hupata changamoto nzuri ya kuiga viranja wao.

### Mazingira Bora ya Ujifunzaji

Mazingira bora ya ujifunzaji yana sifa ya mazingira faafu yenye kujihisi kama jamii moja, matarajio ya juu ya kiakademia na mahusiano chanya miongoni mwa wanafunzi na walimu. Wanafunzi sasa wamewezeshwa kutangamana na nyenzo na raslimali mbalimbali za kielimu na uongozi wa shule. Utamaduni wa shule unapaswa kuwa wa shule iliyo salama, yenye kuunga mkono na kukaribisha kujifunza (Spiro, 2013). Wanafunzi huhitaji pahali salama ili waweze kuendeleza uwezo wao shuleni (Barkman, 2015). Mazingira chanya na mazuri yenye wanafunzi kujihisi salama na wenye kuthaminiwa yameweza kuangaziwa na uongozi wa shule hii.

### Ugatuzi wa Mamlaka

Kiongozi mzuri ni yule ambaye ana imani kwa ugawaji wa majukumu. Shule ni taasisi rasmi inayoongozwa na wasimamizi tofauti wa kielimu kwa viwango tofauti kwa malengo tofauti (Mshelia & Olukayode, 2022). Kila mmoja ana nafasi tosha ya kutekeleza majukumu yake. Kiongozi huyu ni mshirikishi wa walimu wake katika ulingo wa uongozi. Walimu wake wana nafasi bora ya kushiriki katika uongozi wa shule. Uongozi wa shule hii

ya Mungakha unaendeshwa na mwalimu mkuu akisaidiwa na naibu wake. Pia, kuna mwalimu mwandamizi ambaye anafanya kazi pamoja na wakuu wa majopo tofauti kama vile: Mkuu wa jopo la Kiswahili, mkuu wa jopo la Sayansi, mkuu wa jopo la Hisabati, mkuu wa jopo la Kiingereza na mkuu wa jopo la Somo la Kijamii. Vile vile, kuna mkuu wa jopo la michezo, mkuu wa jopo la ushauri nasaha na mkuu wa jopo la usafi wa mazingira.

**Kushirikishwa kwa Wanafunzi**

Shule hii ina utamaduni wa kuhusisha wanafunzi wake katika uongozi wake ili kuwapa nafasi za kukuza vipawa vyao vya uongozi. Viranja huwa na majukumu tofauti katika shule mbalimbali, Shule ya Msingi ya Mungakha ikiwa mojawapo. Majukumu ya viranja yalikuwa ni kusimamia wanafunzi wenzao katika kufanya kazi mbalimbali, kutoa adhabu, kupatanisha walimu na wanafunzi wenzao na kuhakikisha sheria za shule zinafuatwa (Muli, 2011). Nafasi hizi za uongozi kwa wanafunzi zilikuwa msingi wa kupata tajriba ya kuwa viongozi katika umri mdogo na hatimaye kukuza vipawa vyao vya uongozi kwa siku za usoni katika jamii (Kilee, 2015). Uongozi wa wanafunzi ulishirikisha viranja wakuu wawili, mvulana na msichana na viranja wa madarasa wawili kuwakilisha jinsia zote mbili. Vilevile, kuna viranja wawili wawili wanaosimamia michezo na usafi wa mazingira. Kugawa huku kwa mamlaka kwa afisi tofauti na kila mmoja akiwa na nafasi wazi ya utendakazi ni mojawapo ya utamaduni wa uongozi katika shule hii.

**Kuhusisha Wazazi kwa Mipango ya Shule**

Wazazi katika taasisi yoyote ya elimu ni mojawapo ya washikadau wa kimsingi katika uongozi. Wazazi wanapohusishwa moja kwa moja na masomo ya watoto wao, wanafunzi hao wana uwezekano mkubwa wa kupata alama za juu, mahudhurio mazuri ya shule na kuwa na umotishaji wa kiwango cha juu shuleni (Henderson & Mapp, 2002). Jukumu la mwalimu mkuu ni muhimu katika kuwashirikisha wazazi katika kutekeleza na kuendeleza suluhu zihusishazo ushirikiano na wazazi pamoja na kuwepo kwa manufaa ya utangamano wa kijamii na wanajamii (Mleczko & Kington, 2013). Uongozi wa shule hii ulikuza mazingira mema yaliyowakaribisha wazazi; kulikuwa na mawasiliano ya mara kwa mara na nafasi kutolewa kwa wazazi kuhusishwa katika shughuli mbalimbali za shule. Wazazi hawa walihusishwa katika mchakato mzima wa ujifunzaji wa watoto wao. Uongozi wa shule pia uliwahusisha katika miradi mbalimbali ya miundo msingi ya shule. Tena, wazazi walishirikishwa moja kwa moja katika nidhamu ya watoto wao. Wazazi walipohusishwa na uongozi wa shule hii ya Msingi ya Mungakha, kulikuzwa mazingira yenye kumuunga mkono mwanafunzi na kusababisha ufanisi.

**Mawasiliano**

Uongozi huu uliboresha mawasiliano katika Shule ya Msingi ya Mungakha kati yake na wanafunzi, wafanyakazi, walimu na washikadau wengineo. Ni maarifa ya msimamizi ya kuwasiliana ambayo huwatia motisha na kuwapa msukumo wafanyakazi wenzake kufanya kazi kwa bidii ili kuafikia malengo ya kikundi na shirika kwa jumla (Luthra & Dahiya, 2015). Mawasiliano humfanya kiongozi kufanikiwa kwa kukuza viwango bora vya uelewa, utendakazi na mahusiano bora kati ya uongozi na wafanyakazi na hivyo kupelekea matokeo mazuri (Luthra et al., 2015). Uongozi wa shule uliwasiliana kwa njia ya moja kwa moja kati ya wanafunzi na walimu. Vilevile, kulikuwepo na mawasiliano ya wazi kati ya wafanyakazi wa shule kuhusiana na majukumu na matarajio kutokana na utendakazi wao. Hatimaye, uongozi wa shule pia uliwasiliana vyema na washikadau tofauti kama vile wazazi na jamii kwa jumla kuhusiana na shughuli tofauti za shule. Mawasiliano haya kati ya uongozi wa shule na washikadau tofauti yaliwahusisha na kuwashirikisha moja kwa moja katika uongozi wa shule.

Hatimaye, ilibainika wazi kwamba utamaduni wa uongozi katika Shule ya Msingi ya Mungakha ulikuwa wa umoja, uongozi wa kielelezo na ule wa mazingira bora ya ujifunzaji. Utamaduni wa uongozi pia ulijitokeza kupitia ugatuzi wa mamlaka na uongozi, kushirikishwa kwa wanafunzi katika uongozi, kuhusishwa kwa wazazi katika masomo ya wanafunzi na mawasiliano na washikadau tofauti.

**Matumizi ya Kiswahili katika Ujenzi wa Utamaduni wa Uongozi katika Shule ya Msingi ya Mungakha**

Sehemu hii ilishughulikia tathmini ya kiwango cha matumizi ya Kiswahili katika ujenzi wa utamaduni wa uongozi wa Shule hii ya Msingi ya Mungakha. Kiswahili katika shule hii kilikuwa na nafasi kubwa katika kujenga utamaduni wa uongozi. Shule hii ipo katika

kaunti ndogo ya Navakholo, Kaunti ya Kakamega. Eneo hili ni eneo ambalo kwa idadi kubwa ni la wazungumzaji wa lugha ya Kibantu na hivyo lugha ya Kiswahili inakubalika na jamii kwa urahisi. Vilevile, walimu katika shule hii wanatoka katika jamii tofauti na hivyo lugha ya Kiswahili ina nafasi kubwa katika mawasiliano yao ya kila siku. Matumizi ya lugha ya Kiswahili katika ujenzi wa utamaduni wa uongozi yaliangaziwa kwa kuongozwa na kipimo cha Likert kwa kurejelea vigezo vitano: Juu sana, juu, wastani, chini na chini sana. Kiswahili hivyo basi kilitumika katika viwango tofauti kama ifuatavyo:

**Sera ya Lugha**

Sera ya lugha ilikuwa mojawapo ya kiambajengo muhimu kilichoelekeza matumizi ya lugha katika Shule ya Msingi ya Mungakha. Sera ya lugha ilihakikisha matumizi ya lugha ya Kiswahili na Kiingereza kwa kiwango kizuri sana. Viongozi, walimu, wafanyakazi na wanafunzi walitumia lugha ya Kiingereza siku ya Jumatatu hadi Jumatano. Lugha ya Kiswahili nayo ilitumika kuanzia siku ya Alhamisi hadi Jumamosi. Sera hii ilikuwa nguzo kuu kwa viongozi kwa vile walihitajika kuwa kielelezo katika kuendeleza sera hii ya lugha.

Gwaride la lugha iliyotumiwa lilidhibitiwa na sera ya lugha. Siku ya Jumatatu ni siku ya Kiingereza. Siku hii Kiswahili kilitumika kwa kiwango cha chini sana. Mwalimu mkuu aghalabu huchanganya Kiswahili na Kiingereza huku akitumia Kiswahili kwa kiwango cha chini sana katika hotuba yake. Naibu wake mara nyingi hujipata akitumia Kiingereza kwa kiwango kikubwa sana ikilinganishwa na Kiswahili anachokitumia kwa wastani. Hata hivyo, mwalimu mwandamizi ambaye ni mwalimu wa Kiswahili naye hukiuka sera ya lugha kwa kutumia Kiswahili zaidi siku zote za gwaride. Kwa upande wa viranja, siku ya Jumatatu wao hujikita kwa lugha ya Kiingereza kwa kiwango cha juu sana kinyume na walimu ambao huwa huru kuchagua lugha ya kutumia.

Siku ya Ijumaa sera ya lugha ilielekeza matumizi ya lugha ya Kiswahili. Viongozi wote hutumia lugha ya Kiswahili kwa kiwango kizuri sana katika mawasiliano yote kwenye gwaride. Kiswahili kilitumiwa zaidi huku Kiingereza kikijitokeza kwa kiwango cha chini sana. Walimu walijitahidi kuzungumza kwa Kiswahili kwa kiwango kizuri bila changamoto kutokana na wote kuandaliwa kufundisha masomo yote, somo la Kiswahili likiwa mojawapo. Viranja vilevile, hususan wale walio kwenye zamu na kiranja mkuu, walihutubia kwa lugha ya Kiswahili. Hivyo basi, Kiswahili hutumika kwa kiwango kizuri sana na uongozi katika kuhutubia wanafunzi katika gwaride.

**Mikutano Rasmi ya Shule**

Mikutano rasmi ya shule kama vile mikutano ya walimu mwanzoni mwa muhula na mwishoni mwa muhula ilikuwa sehemu ya utamaduni wa shule. Vilevile, kulikuwepo na mikutano ya majopo tofauti iliyoongozwa na mkuu wa jopo na kuhusisha wanajopo. Hatimaye, kulikuwepo na mikutano ya uongozi wa shule pamoja na wanajopo na wakuu wa idara nyinginezo kama vile za michezo na ushauri nasaha. Lugha ya Kiingereza ndiyo ambayo ilitawala mikutano hii kwa kutumika kwa kiwango kikubwa sana. Kutokana na urasmi wa masuala yanayowasilishwa, Kiswahili hakitumiki katika mikutano hiyo ila tu wakati ambapo mkuu wa jopo la Kiswahili ndiye anawasilisha. Hivyo basi, Kiswahili hutumika kwa kiwango cha chini katika mikutano mbalimbali ya walimu katika kila muhula.

**Mikutano ya Wazazi**

Shule hii ya Msingi ni shule ambayo iko katika mazingira ya kijijini hii ikiwa sababu mojawapo ya kiwango chao cha chini cha elimu. Mikutano ya wazazi katika shule hii huendeshwa katika lugha ya Kiswahili. Hali hii ililazimu matumizi ya Kiswahili huku ikiwa vigumu kuwasiliana kwa Kiingereza. Hata hivyo, Kiingereza kilitumika kwa kiwango cha chini huku maelezo hayo hayo yakitolewa tena kwa Kiswahili. Vilevile, kutokana na idadi kubwa ya walimu kutoka katika jamii tofauti na hivyo si wenyeji wa jamii hii, Kiswahili kilitumika licha ya baadhi ya wazazi kupendelea lugha asilia kutumiwa katika mawasiliano. Lugha asilia ilitumika kwa kiwango cha wastani katika mikutano ya wazazi. Lugha asilia ilikuwa muhimu katika kupitisha sera za shule na uongozi wa shule kwa wazazi. Lugha, hususan ya Kinyala, ilitumika katika kutoa ufafanuzi na pia kwa mawasiliano kutoka kwa wazazi walipojieleza kwa usimamizi wa shule.

**Lugha ya Uongozi Afisini**

Uongozi huu wa shule katika kuendeleza majukumu yake ulihitajika kuwasiliana na washikadau tofauti afisini. Mwalimu mkuu, naibu wake na mwalimu mwandamizi waliwasiliana na walimu wenzao,

wanafunzi na wafanyakazi wa shule kila uchao afisini. Vilevile, mara kwa mara walitembelewa na washikadau tofauti kama vile wazazi na wageni wengine mbalimbali. Viongozi wa shule hii ya Msingi ya Mungakha walikitumia Kiswahili kwa kiwango kikubwa. Kiswahili kilitumika kama lugha rasmi katika afisi ya mwalimu mkuu, naibu wake au mwalimu mwandamizi walipotembelewa na wazazi. Mara kwa mara wazazi walipokuja afisini kwa huduma mbalimbali, lugha ya Kiswahili ilitumika katika kutoa huduma hizo. Wengi wa wazazi hao walikitumia Kiswahili kuwasiliana na mwalimu mkuu, huku wachache wakitumia Kiingereza. Vilevile, lugha ya mama ilitumika kwa kiwango cha chini sana katika mawasiliano katika afisi na viongozi katika shule ya Mungakha. Lugha hii ya Kinyala ilitumika hasa na wazazi wenye umri mkubwa.

**Mikutano ya Wafanyikazi**

Mikutano ya wafanyakazi pia ni mikutano muhimu sana katika shule yoyote. Mikutano hii ilikuwa muhimu katika kuratibu utendakazi wa wafanyakazi katika shule hii. Mikutano hii huendeshwa zaidi kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Hii ni kwa sababu kiwango cha elimu cha baadhi ya wafanyakazi ni cha chini na hivyo hawachangamkii matumizi ya lugha ya Kiingereza katika mikutano yao. Hata hivyo, lugha ya Kiingereza hutumika pia japo si sana. Vilevile, lugha ya mama pia ilitumika kwa kiwango cha chini. Kwa sababu hii, lugha ya Kiswahili ndiyo inayotumika zaidi katika mawasiliano kwenye mikutano yao.

**Mikutano ya Darasa**

Mikutano ya darasa inayofanyika kila juma pia ni sehemu muhimu kwa walimu wa darasa kutangamana na wanafunzi wao. Mikutano hii hurejelea masuala yanayoibuka kila siku huku mengi yayo yakitatuliwa papo hapo. Kiswahili kilitumika kwa kiwango kikubwa sana katika mikutano hii ya darasa. Walimu wa darasa kuanzia darasa la kwanza hadi la nne walikiri kuwa Kiswahili kilitumika kwa kiwango kikubwa. Lugha ya Kiingereza ilitumika kwa kiwango kizuri kati ya darasa la kwanza hadi la nne, huku Kiingereza kikitumika kwa kiwango kizuri sana kati ya darasa la tano hadi la nane. Lugha ya Kiswahili ilitumika katika kiwango kizuri sana kutekeleza sera ya lugha, mikutano ya wazazi na mikutano ya darasa la kwanza hadi la nne. Kiingereza pia kilitumika kwa kiwango kizuri sana katika kutekeleza sera ya lugha, mikutano rasmi ya shule na mikutano ya darasa la tano hadi la nane. Kisha, Kiswahili kilitumika katika kiwango kizuri katika lugha ya uongozi, mikutano ya wafanyakazi na mikutano ya darasa la tano hadi la nane. Kiingereza vilevile kilitumika kwa kiwango kizuri katika mikutano ya darasa la kwanza hadi la nne, nayo lugha ya Kinyala katika mikutano ya wazazi. Vilevile, Kiswahili kilitumika katika kiwango cha chini katika mikutano rasmi ya shule. Kiingereza nacho kilitumika katika kiwango cha chini katika mikutano ya wazazi na lugha ya uongozi afisini. Wafanyakazi wa shule walitumia lugha ya Kiingereza kwa kiwango cha wastani katika mikutano yao. Hatimaye, lugha ya Kinyala ilitumika katika kiwango cha chini sana katika mikutano ya wafanyakazi na katika kuwasiliana na viongozi afisini.

**Mitazamo ya Washikadau Kuhusu Matumizi ya Kiswahili katika Uongozi wa Shule ya Msingi ya Mungakha**

Shule hii ya Msingi ya Mungakha ina washikadau tofauti. Washikadau kwa muktadha wa utafiti huu walihusisha walimu, wafanyakazi, halmashauri ya shule, viranja na wanafunzi. Uongozi wa shule hii ulihusisha halmashauri ya shule, wanafunzi, wakuu wa majopo tofauti shuleni, mwalimu mwandamizi, mwalimu mkuu na naibu wake. Washikadau hawa walikuwa na mitazamo chanya kuhusu matumizi ya Kiswahili katika uongozi wa shule. Mitazamo hii ilikuwa kama ifuatavyo;

**Mtazamo wa Wanafunzi kuhusu Matumizi ya Kiswahili**

Wanafunzi walikuwa na mtazamo chanya kuhusu matumizi ya Kiswahili na uongozi wa Shule ya Mungakha. Mtazamo wa wanafunzi kuhusu matumizi ya Kiswahili ulikuwa wa kiwango cha juu. Mara nyingi mwalimu mkuu alipozungumza kwa Kiswahili wanafunzi walichangamkia ujumbe wake. Hali hii ilikuwa vivyo hivyo kwa naibu wa mwalimu mkuu na mwalimu mwandamizi. Wanafunzi vilevile walifurahia viranja walipowaelekeza na kuwasiliana nao kwa lugha ya Kiswahili. Wanafunzi walifurahia matumizi ya Kiswahili kwa kiwango cha juu. Hata hivyo, mtazamo wao kwa matumizi ya lugha ya Kiingereza ulikuwa wa kiwango cha chini. Wanafunzi, hasa wale wa darasa la kwanza hadi la tano, hawakuchangamkia matumizi ya lugha ya Kiingereza na walifurahia matumizi ya Kiswahili.

**Mtazamo wa Wanafunzi kwa Walimu wa Darasa**

Vilevile, wanafunzi pia walikuwa na mwelekeo chanya kwa walimu wa darasa walipoendesha mikutano ya darasa kwa lugha ya Kiswahili. Lugha ya Kiswahili ilikuwa rahisi kueleweka ikilinganishwa na Kiingereza. Mtazamo wa wanafunzi kuhusu matumizi ya Kiswahili na walimu wa darasa ulikuwa ni wa kiwango cha juu sana. Wanafunzi walichangia kwa haraka mijadala darasani na pia kuibua masuala mbalimbali wanayokumbana nayo kila siku. Kwa upande mwingine, wanafunzi walikuwa na mtazamo wa kiwango cha wastani kuhusu matumizi ya lugha ya Kiingereza. Kiingereza kilisisitizwa kutumiwa na wanafunzi kati ya darasa la tano hadi la nane huku madarasa mengine yakipendelea matumizi ya Kiswahili.

**Mtazamo wa Wazazi kuhusu Matumizi ya Kiswahili**

Wazazi wa shule hii ya Msingi pia walikuwa na mwelekeo chanya kuhusu matumizi ya Kiswahili na uongozi wa shule. Mtazamo wa wazazi katika matumizi ya Kiswahili ulikuwa chanya sana. Kwanza, mara nyingi wengi wa wazazi hawa walitumia lugha ya Kiswahili kila walipomtembelea mwalimu mkuu, naibu wake ama mwalimu mwandamizi shuleni. Pia, wazazi walifurahia matumizi ya Kiswahili katika mikutano ya wazazi. Wazazi waliuchukulia uongozi wa shule kama sehemu yao kwa vile Kiswahili kiliwawezesha kuwasiliana nao moja kwa moja kinyume na iwapo wangewasiliana kwa lugha ya Kiingereza. Hata hivyo, mtazamo wa wazazi kuhusu matumizi ya lugha ya Kiingereza ulikuwa si chanya. Baadhi ya wazazi walikitumia Kiingereza katika kujieleza na walifurahia kilipotumika. Kwa upande mwingine, wazazi wachache sana walifurahia matumizi ya lugha ya mama. Hii ni kwa sababu walihisi kuwa hiyo ilikuwa ni ishara kuwa walikuwa shuleni kinyume na pale walipohutubiwa kwa lugha mama kwingineko.

**Mtazamo wa Wafanyikazi wa Shule Kuhusu Lugha ya Kiswahili**

Wafanyakazi wa shule pia walikuwa na mwelekeo chanya kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili katika shule hii. Mtazamo wa wafanyakazi kuhusu lugha ya Kiswahili ulikuwa chanya katika mikutano, mawasiliano au kutoa ripoti kwa mwalimu mkuu. Matumizi ya lugha ya Kiswahili yalikuwa mwafaka kwa vile waliweza kujieleza vyema kinyume na iwapo wangetumia lugha ya Kiingereza. Vilevile, Kiswahili kiliwawezesha kupata mawasiliano na ripoti kutoka kwa uongozi kwa wepesi sana. Wafanyakazi katika kuwasilisha ripoti tofauti pia walijihisi huru walipotumia lugha ya Kiswahili. Kwa sababu hiyo, nyingi ya ripoti za wafanyakazi kwa mwalimu mkuu au naibu wake zilitolewa kwa Kiswahili mwishoni mwa siku, juma na wakati mwingine mwezi. Vilevile, wafanyakazi hawa walikuwa na mtazamo hasi kuhusu matumizi ya Kiingereza. Walikitumia Kiingereza kwa kiwango cha chini katika kuwasilisha ripoti zao na katika mawasiliano yao ya mara kwa mara.

**Mtazamo wa Walimu wa Shule ya Msingi ya Mungakha kwa Lugha ya Kiswahili**

Walimu walikuwa na mtazamo chanya kuhusu matumizi ya Kiswahili na uongozi katika shule hii ya Msingi. Mtazamo wa lugha ya Kiswahili ulikuwa wa kiwango cha juu sana kwa jumla katika shule hii. Lugha hii ya Kiswahili ilitumika kwa miktadha rasmi kama vile mikutano na gwaride hususan siku ya Ijumaa. Walimu walikuwa na mtazamo chanya kwa matumizi ya Kiswahili na uongozi wa shule. Tena, walimu walikuwa na mtazamo chanya Kiswahili kilipotumika kwa mikutano isiyo rasmi kama vile katika gumzo na maongezi ya kawaida kati ya mwalimu mkuu na walimu wenzake. Hii ilitokana na walimu wake kuwa wa makabila tofauti. Isitoshe, wote waliandaliwa kukifundisha Kiswahili. Hata hivyo, lugha ya Kiingereza pia ilitumika kwa kiwango kikubwa. Sera ya lugha ilipendelea matumizi ya lugha ya Kiingereza kwa kutumiwa siku tatu kuanzia Jumatatu hadi Jumatano. Hali hii ilikuwa kinyume na lugha ya Kiswahili iliyotengewa siku mbili japo ilichangamkiwa zaidi na walimu.

**Mtazamo wa Halmashauri ya Shule ya Msingi ya Mungakha**

Halmashauri ya shule ni mojawapo ya kiambajengo kikuu cha uongozi katika shule yoyote ile. Hali hii si tofauti na Shule ya Msingi ya Mungakha. Halmashauri ya shule hii ilikuwa na mtazamo wa kiwango cha wastani kuhusiana na matumizi ya lugha ya Kiswahili. Hali hii ilitokana na wengi wao kuwa wasomi katika taaluma mbalimbali. Hata hivyo, walikuwa na mtazamo chanya sana kwa Kiingereza kutokana na kiwango chao cha juu cha masomo. Halmashauri hii ya shule ilikuwa na mapendeleo kwa matumizi ya lugha ya Kiingereza ilhali Kiswahili na Kiingereza zote ni lugha rasmi nchini Kenya.

Hatimaye, mitazamo ya washikadau kuhusu matumizi ya Kiswahili katika uongozi ilitofautiana miongoni mwa washikadau kama ifuatavyo: Mtazamo wa kiwango kizuri sana ulijitokeza katika wanafunzi kuwarejelea walimu wao wa darasa katika matumizi ya Kiswahili. Walimu wa shule hii pia walikuwa na mtazamo wa kiwango kizuri sana kuhusiana na matumizi ya lugha ya Kiswahili. Vilevile, halmashauri ya shule hii pia ilikuwa na mtazamo wa kiwango cha juu sana katika kurejelea matumizi ya lugha ya Kiingereza. Zaidi ya hayo, mtazamo wa kiwango cha juu ulijitokeza kwa kurejelea matumizi ya Kiswahili kutoka kwa wanafunzi shuleni, wazazi na wafanyakazi wa shule.

Huku walimu wakiwa na mtazamo wa kiwango cha juu kwa kurejelea lugha ya Kiingereza ilipotumiwa katika shule hii ya Msingi ya Mungakha. Halmashauri ya Shule hii ya Msingi ya Mungakha ilikuwa na mtazamo wa kiwango cha wastani kurejelea lugha za Kiingereza na Kiswahili zilivyotumika katika uongozi. Tena, wanafunzi wakiwarejelea walimu wao wa darasa walikuwa na mtazamo wa kiwango cha wastani kurejelea walivyotumia lugha za Kiswahili na Kiingereza mtawalia. Wafanyakazi wa shule na wazazi nao walikuwa na mtazamo wa kiwango cha chini kwa kurejelea matumizi ya lugha ya Kiingereza. Mwishowe, wazazi wa shule hii ya Msingi ya Mungakha walikuwa na mtazamo wa kiwango cha chini kuhusu matumizi ya lugha asilia ya Kinyala.

**HITIMISHO NA MAPENDEKEZO**

**Hitimisho:** Makala haya yamebainisha kuwa Kiswahili kilikuwa na nafasi kubwa katika ujenzi wa utamaduni wa uongozi katika Shule ya Msingi ya Mungakha. Utamaduni katika shule hii ulikuwa wa umoja, uongozi wa kielelezo, mazingira bora ya ujifunzaji, ugatuzi wa mamlaka, kushirikishwa kwa wanafunzi, kuhusishwa kwa wazazi na mawasiliano. Lugha ya Kiswahili na Kiingereza zilitumika kwa kiwango kizuri katika ujenzi wa utamaduni wa uongozi. Hata hivyo, lugha ya Kinyala nayo ilitumika katika kiwango cha chini katika ujenzi wa utamaduni wa uongozi. Washikadau katika Shule ya Msingi ya Mungakha walikuwa na mtazamo wa kiwango cha juu kuhusu lugha ya Kiswahili, mtazamo wa kiwango cha wastani kwa kurejelea lugha ya Kiingereza na mwishowe mtazamo wa kiwango cha chini sana kuhusu matumizi ya lugha ya Kinyala katika shule hii.

**Mapendekezo:** Haja ipo ya utafiti zaidi kufanywa kwa kurejelea sio tu shule za msingi bali pia shule za upili na vyuo vikuu. Vilevile, tafiti zaidi zifanywe sio tu kwa kurejelea uongozi bali pia viongozi wa ngazi tofauti. Tafiti pia zifanywe kurejelea nafasi ya lugha nyinginezo kama vile lugha asilia katika ujenzi wa utamaduni wa uongozi katika taasisi mbalimbali za elimu. Aidha, tafiti zilenge pia maeneo ya mijini kinyume na utafiti huu ambao ulilenga shule ya kijijini.

**MAREJELEO**

Aibieyi, S. (2014). Approaches, skills and styles of leadership in organizations. *Review of Public Administration and Management, 3*(5), 53–59. Retrieved from Arabian Journal of Business and Management Review

Allport, G. W., & Odbert, H. S. (1936). *Trait-names: A psycho-lexical study*. *Psychological Monographs, 47*(1), 1–170.

Barkman, C. (2015). The characteristics of an effective school leader. *BU Journal of Graduate Studies in Education, 7*(1), 14–18. Retrieved from ERIC

Block, L. (2003). The leadership culture connection: An exploratory investigation. *Leadership & Organization Development Journal, 24*(6), 318–334. https://doi.org/10.1108/01437730310494293

Buenviaje, M. G., Refozar, R. F. G., Encio, A. H., Perez, M. P., & Laguador, J. M. (2017). Leader motivating language affecting faculty members' work performance from a private academic institution in the Philippines. *Asia Pacific Journal of Education, Arts and Sciences, 4*(3), 121–130. Asia Pacific Journal of Education, Arts and Sciences

Case, P., Connell, G. J., & Jones, J. M. (2017). The language of leadership in Laos. *Leadership, 13*(2), 173–193. https://doi.org/10.1177/1742715016658214

Daoud, J., & Tarek, M. (2023). The role of leadership in changing organizational culture. *Social Science Research Network Journal, 1*(3), 24–37.

Fleenor, J. W. (2006). *The SAGE encyclopedia of industrial and organizational psychology* (2nd ed.). Sage Publications.

Henderson, A., & Mapp, K. L. (2002). *A new wave of evidence: The impact of school, family and community connections on student achievement*. Southeast Educational Development Laboratory.
Hongboontri, C., & Keawkhong, N. (2014). School culture: Teachers' beliefs, behaviors and instructional practices. *Australian Journal of Teacher Education, 39*(5), 66–88. Australian Journal of Teacher Education
Kilee, M. M. (2015). *The role of prefects in management of secondary schools: A case study of Kandara Division; Maragua District* (Unpublished master's thesis). Kenyatta University.
Luthra, A., & Dahiya, R. (2015). Effective leadership is all about communicating effectively: Connecting leadership and communication. *International Journal of Management & Business Studies, 5*(1), 43–48.
Mahamed, H. M. (2015). *Perceptions of stakeholders on Somali language as a medium of instruction in public primary school in Benadir Region, Mogadishu, Somalia* (Unpublished master's thesis). The University of Nairobi.
Misheck, D. I., & Shoko, Y. (2013). Stakeholders perception of the language of instruction policy in Malawian primary school and its implications for the quality of education. *International Household Survey Network, 1*(1), 155–165. International Household Survey Network
Mleczko, A., & Kington, A. (2013). The impact of school leadership on parental engagement: A study of inclusion and cohesion. *International Research in Education Journal, 1*(1), 129–148.
Mshelia, H. J., & Olukayode, E. (2022). Leadership styles and their applications for effective school administration. *International Journal of Scientific and Management Research, 5*(2), 56–63. https://doi.org/10.37502/IJSMR.2022.5205
Muli, M. W. (2011). *The role of prefects in the governance of public secondary schools in Machakos Central Division, Machakos District, Kenya* (Unpublished master's thesis). Kenyatta University.
Mwakale, C. H. W. (2017). *Leadership and quality culture in private universities in Kenya: A case of Marist International University College* (Unpublished master's thesis). Kenyatta University.
Nahame, Y. U., Baba, A. I., & Abdullahi, A. (2015). The role of unity and effective leadership in community development. *International Journal of Engineering, Management and Social Sciences Paradigm, 17*(1), 1–5.
Punch, K. F. (2013). *Introduction to social research: Quantitative and qualitative approaches*. Sage Publications.
Santri, R. P. (2016). Hubungan kepemimpinan kepala sekolah dan budaya sekolah dengan kinerja guru SD Negeri di Kota. *Manajer Pendidikan, 10*(3), 74–86.
Sealy, R., & Singh, V. (2008). The importance of role models in the development of leaders' professional identities. In K. James & J. Collins (Eds.), *Studying leadership* (pp. 208–222). Palgrave Macmillan.
Souba, W. W., & Souba, M. H. (2016). Leadership and the limitation of language. *Open Journal of Leadership, 5*, 39–50. https://doi.org/10.4236/ojl.2016.52005
Spiro, J. D. (2013). Effective principals in action. *Phi Delta Kappan, 94*(8), 27–31.
Tampubolon, M., & Harati, H. (2019). Role of organizational culture, communication and leadership style on job satisfaction. *International Journal of Research in Business and Social Science, 8*(5), 308–315.
Tembe, J., & Norton, B. (2008). Promoting languages in Ugandan primary schools: The community as stakeholders. *Canadian Modern Language Review, 65*(1), 33–60.
Usman, N., & Yusrizal, M. (2016). Pengembangan budaya sekolah untuk peningkatan kompetensi profesional guru pada MTsN 1 Takengon. *Jurnal Magister Administrasi Pendidikan, 4*(4), 42–51.
Widodo, H. (2019). The role of school culture in holistic education development in Muhammadiyah Elementary School Sleman Yogyakarta. *Dinamika Ilmu, 19*(2), 265–285.
Xenikou, A. (2022). Leadership and organizational culture. In C. Newton & R. Knight (Eds.), *Handbook of research methods for organizational culture* (pp. 23–38). Edward Elgar Publishing. https://doi.org/10.4337/9781788976268.00009